



**MAFUNZO YA WALIMU KAZINI NGAZI YA SHULE  
KWA MWALIMU WA DARASA LA I-III**

**Moduli ya Kumi na Mbili:**  
KUSOMA KWA UFAHAMU

**Mwongozo wa Mratibu  
wa Mafunzo ya Walimu  
Kazini Ngazi ya Shule**



**Moduli hii imetayarishwa kwa ushirikiano na:**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi  
Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa  
Taasisi ya Elimu Tanzania  
Chuo Kikuu cha Dodoma  
Chuo cha Ualimu Morogoro  
Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam  
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania  
Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa  
EQUIP-Tanzania

**Moduli hii imewezeshwa kwa ushirikiano na:**

C.C.U Butimba  
C.C.U Bustani  
C.C.U Tabora  
C.C.U Ndala  
C.C.U Kasulu  
C.C.U Kabanga  
C.C.U Bunda  
C.C.U Tarime  
C.C.U Shinyanga  
C.C.U Mpwapwa



## **Maelezo Muhimu kwa Mratibu wa Mafunzo ya Walimu Kazini Ngazi ya Shule**

Mwongozo huu utatumika sanjari na moduli ya kumi na mbili ya mwalimu ili kumsaidia mratibu wa mafunzo kuwa na mpangilio mzuri wenye kufuata hatua kwa hatua ili kuwafanya walimu washiriki kikamilifu katika kujifunza maudhui ya moduli ya kumi na mbili .

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ambayo ni upande wa kushoto wa mwongozo unabeba maelezo ambayo mratibu wa mafunzo ya walimu kazini ngazi ya shule atatakiwa kuyafuata wakati wa kuratibu kipindi cha kujifunza maudhui ya moduli. Sehemu ya pili ambayo ni upande wa kulia wa mwongozo unabeba maudhui yaliyo kwenye moduli ya mwalimu ambayo watayasoma wakati wa kipindi cha kujifunza.

Wakati wa kipindi cha kujifunza, unatakiwa kufuata maelezo yanayokuongoza yaliyo upande wa kushoto wa mwongozo huu na kuyahusianisha na maudhui yaliyo kwenye moduli ya mwalimu ambayo yapo upande wa kulia wa mwongozo huu kama yanavyosomeka kwenye moduli ya mwalimu.

## MAELEKEZO NA TASWIRA KATIKA MODULI

Kuna picha na michoro mingi katika moduli. Baadhi zinajirudia mara nyingi kwa sababu zinamaanisha jambo mahususi linalotokea. Zifuatazo ni mifano ya taswira mbalimbali ambazo zinapatikana katika moduli pamoja na kile ambacho zinawakilisha:



**Jadili na mwenzako:** Wakati wote wa kusoma moduli, walimu wataelezwa kufanya kazi pamoja na mwalimu mwingine juu ya maswali au kazi.



**Fikiri- Wawili wawili – Shirikishana:** Kama ilivyo katika maelezo ya hapo juu, hapa vilevile walimu wanafanya kazi wakiwa wawili wawili. Japokuwa, hapa walimu wanatafakari mmoja mmoja kwanza juu ya swali au tatizo, halafu mwalimu anafanya kazi na mwenzake na mwishoni wanawasilisha katika kundi lote.



**Jadiliana katika kikundi:** Wakati mwingine walimu wataelekezwa kutafakari au kujadili maswali mbalimbali katika kikundi.



**Soma:** Katika kila moduli kuna “dhana kuu” ambayo kwa kawaida huwasilishwa kwa kirefu katika maelezo.



**Andika:** Moduli itawahamasisha walimu kuchukua maelezo na kuandika fikra zao na majibu.



**Igizo:** Baadhi ya mazoezi yatahitaji walimu kuigiza kazi ya KUFUNDISHA wakati wengine watapaswa kuigiza kama wanafunzi.

## MAELEKEZO KWA MRATIBU WA MAFUNZO YA WALIMU KAZINI

Kabla ya kuanza moduli hii, angalia 'maelekezo muhimu' na hakikisha kuwa wewe na walimu mnayatekeleza.

Tafadhali waambie walimu wajiorodheshe na kusaini hapa chini.

Tarehe:	Shule:	Wilaya:	Mkoa:
Muda wa kuanza:	Jina la Mratibu na sahihi yake:		
Muda wa kumaliza:	Jina la Mwalimu Mkuu na sahihi yake:		

	JINA LA MWALIMU	ME / KE	SAHIHI:	DARASA
1				
2				
3				
4				
5				
6				
7				
8				



### WAAMBIE WALIMU:

**“Sasa tutasoma utangulizi wa moduli hii. Tutasoma matini kwa sauti na kwa kupokezana. Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma aya ya kwanza, atamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome aya inayofuata.”**

## MODULI YA 12: KUSOMA KWA UFAHAMU

### MAUDHUI YA MODULI

Moduli ya 5 – 8 inahusu dhana na mbinu za KUFUNDISHA kusoma ambazo zinaendana na mabadiliko yaliyo kwenye muhtasari mpya wa darasa la kwanza na la pili. Moduli hii pia inahusu baadhi ya dhana na shughuli kama zilivyoanishwa kwenye muhtasari mpya wa darasa la kwanza na la pili. Moduli hii inahusu **kusoma kwa ufahamu**, au uwezo wa mwanafunzi wa kufahamu, kufikiria na kujibu swali kuhusu aya (iliyosomwa au aliyosikia). Hii inajumuisha utafutaji wa taarifa katika aya, kufikiria na kufanya uchunguzi kuhusu wahusika, kuhusianisha aya na maisha ya kawaida, na mengine mengi. Kuna **aina nyingi za maswali** ambayo walimu wanaweza kuuliza wanafunzi ili kuwasaidia kuelewa kile walichosikia au kusoma. Baadhi ya maswali ni rahisi kuliko mengine na shurti yote yapangiliwe vizuri ili kuhakikisha kwamba malengo ya kujifunza yanafikiwa.

### DHANA KUU

1. **Maswali yanayojenga kumbukumbu** – Maswali kuhusu mambo ya kweli katika hadithi. Wanafunzi wanaweza kujibu maswali ya juu juu kwa kufuatilia mtiririko wa hadithi. Mara nyingi ni maswali yanayotokana na ukweli katika hadithi na yanakuwa na jibu moja au majibu machache sana.
2. **Maswali yanayofikirisha** – Maswali yanayohitaji wanafunzi wafikirie hadithi katika hali ya juu zaidi ya habari waliyopewa. Mara kwa mara ni maswali yanayouliza “jinsi gani” au “kwanini” na mara nyingi yanahusu motisha au hisia. Maswali ya kina husaidia wanafunzi kuwa hodari na wasomaji makini.
3. **Maswali yanayohusisha uzoefu na mazingira** – Maswali yanayotengeneza muunganiko kati ya kile wanafunzi walichosoma na uzoefu wao binafsi.

### MALENGO YA MODULI

Mwishoni mwa moduli hii, walimu wataweza:

1. Kufahamu jinsi/kwanini aina tofauti za maswali (kabla/wakati wa/baada ya kusoma) yanakuza ufahamu wa kusoma wa mwanafunzi.
2. Kukadiria viwango vya ufahamu vya wanafunzi katika madarasa yao.
3. Kutumia shughuli mbalimbali na mikakati kuimarisha stadi za ufahamu.
4. Kupanga kitabu kikubwa ili kusaidia mbinu mbalimbali za kusoma.

### MAELEKEZO MUHIMU

1. Mara zote njoo na moduli ya mafunzo ya walimu kazini na kalamu.
2. Njoo na kitabu cha hadithi (kama kinapatikana).

### TARATIBU ZA KUJIFUNZA KWA KILA KIPINDI

1. Kutana katika sehemu tulivu yenye ubao kama inavyoonekana katika picha.
2. Panga madawati/meza ili kuwezesha washiriki wote waonane na kuongea kwa pamoja.
3. Waeleze walimu wawe huru kuuliza maswali kama hawajaelewa.
4. Waeleze walimu kuwa msaada kwa wenzao.
5. Waeleze walimu kuwa wabunifu na kufikiria dhana watakazojifunza na jinsi zitavyohusiana na darasa lao.
6. Waeleze walimu waweke simu zao katika hali ya mtetemo.



## TAFAKARI



### WAAMBIE WALIMU:

**“Tangu moduli ya 11, umefanyia mazoezi shughuli mbili kwenye kipindi cha kujifunza kusoma na kuandika. Orodhesha mafanikio uliyoyaona pamoja na changamoto ulizokabiliana nazo wakati wa KUFUNDISHA maudhui ya moduli hiyo darasani kwako. Una dakika 5 kwa ajili ya kazi hii.”**



### WAAMBIE WALIMU:

**“Sasa tutajadili kwa pamoja mafanikio na changamoto katika kikundi. Kwa kila changamoto ambayo imewasilishwa tufikiri kwa pamoja kuhusu namna ya kukabiliana nayo. Kumbuka kuandika ufumbuzi ambao unaweza kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Tutatumia dakika 10 kwa majadiliano.”**



## TAFAKARI

Katika kipindi cha mwisho tulisoma kuhusu **msamiati**. Orodhesha mafanikio uliyoyaona pamoja na changamoto ulizokabiliana nazo wakati wa KUFUNDISHA maudhui ya moduli hiyo darasani kwako.



### ANDIKA PEKE YAKO (DAKIKA 5)

Tafadhali andika kwenye visanduku mafanikio na changamoto ulizokutana nazo wakati wa kutekeleza mikakati hii katika darasa lako.

#### Mafanikio

(Elezea utaratibu uliotumia na fafanua jinsi ulivyofanikiwa)

#### Changamoto

(Elezea utaratibu uliotumia na fafanua changamoto zake)



### JADILIANA KATIKA KIKUNDI (DAKIKA 10)

1. Shirikisha wenzako kwenye kundi mojawapo kuhusu uzoefu huo.
2. Kwa kila changamoto, pendekeza namna ya kukabiliana nayo.
3. Wakati wa majadiliano, andika ufumbuzi unaoendana na changamoto ulizobainisha.

#### Njia Muhimu za Ufumbuzi

(Mawazo muhimu na mahususi kwa wenzetu)

## UTANGULIZI



### WAAMBIE WALIMU:

**Leo, tutaanza kwa kujadili matini fupi. Nitaisoma kwa sauti na pia nitawauliza maswali kadhaa kabla ya kusoma, na baada ya kusoma. Tafadhali jibu maswali yangu vizuri zaidi kwa kadri unavyoweza.**

**Kabla ya kusoma, waulize walimu maswali matatu:**

- 1. Je, ni jina la kiumbe katika kielelezo hiki?**  
(kama waalimu hawajui, jibu sahihi ni: pweza)
- 2. Je, ni aina gani za viumbe wa baharini una uzoefu nao?**  
(hakikisha waalimu wanajibu – majibu yote ni sawa)
- 3. Je, mnafikiri matini hii itakuwa inahusu nini?**  
(hakikisha waalimu wanajibu – majibu yote ni sawa)

**Sawa, sasa naanza kuisoma aya kwa sauti.**

(Baada ya kumaliza, uliza maswali yafuatayo:)

- 1. Je, pweza ana mioyo mingapi?**  
(kama walimu hawajui, jibu ni: 3)
- 2. Je, ni mbinu gani ambazo pweza anazitumia kujinasua kutoka katika hali ngumu?**  
(kama walimu hawajui, jibu ni: kubadili rangi ya ngozi ifanane na mchanga na kunyunyiza wino)
- 3. Kwanini unafikiri mbinu hizi ni za lazima?**  
(kama walimu hawajui, jibu ni: ili kujihami na au kuwakwepa wanyama wanaowinda na kula wenzao)
- 4. Kama binadamu, unazo mbinu ambazo unazitumia kujinasua ukiwa katika hali ngumu?**  
(hakikisha walimu wanajibu)
- 5. Je, pweza ana mikono mingapi?**  
(kama walimu hawajui, jibu ni: 8)
- 6. Kwanini unafikiri wana mikono mingi?**  
(majibu yanaweza kujumuisha: kuogelea haraka, kujisogeza kuzunguka kwenye sakafu ya bahari, kukamata kitoweo, n.k.)
- 7. Je, ulishawahi kuona au kugusa pweza?**  
(hakikisha walimu wanajibu)
- 8. Je, unajua wanyama wengine wowote walio na kiwango cha juu cha akili?**  
(hakikisha waalimu wanajibu – majibu yote ni sawa)
- 9. Je, unaweza kufupisha kwa sauti matini kwa maneno yako mwenyewe?**  
(sharti mwalimu ataje kwamba pweza wana akili)

## UTANGULIZI



### ZOEZI LA KUCHANGAMSHA (DAKIKI 10)

Leo, tutaanza kwa kujadili matini fupi. Mratibu ataisoma kwa sauti na pia atawauliza maswali kadhaa kabla ya kusoma, na baada ya kusoma. Tafadhali jibu maswali yake vizuri zaidi kwa kadri unavyoweza.

### Viumbe visivyo vya kawaida kutoka baharini

Ni kiumbe gani ana mioyo mitatu, mikono nane, na ubongo mkubwa sana? Pweza – ni kiumbe anayeweza kufanya mambo ya kushangaza sana. Pweza wana kiwango cha juu sana cha akili. Wanaweza kujifunza mambo mapya kama vile binadamu. Wamejifunza hata mbinu chache za kujinasua kutoka katika hali ngumu. Pweza wanapenda kujificha kwenye mchanga chini katika sakafu ya bahari. Wanaweza kujibadilisha rangi ya ngozi yake ifanane na mchanga. Kubadilika huku kwa rangi au majificho, hutokea kwa muda chini ya dakika moja. Pweza wanaweza pia kurusha wino mweusi unaochipukia mahali maalumu, na kutengeneza wingu jeusi linalowaficha wakati wanaogelea kuondoka pale walipo.



## DHANA KUU



### WAAMBIE WALIMU:

**“Sasa tutasoma maudhui muhimu. Tutasoma kwa sauti matini kwa kupokezana.**

**Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma aya ya kwanza, utamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome aya inayofuata.**

**Wakati wa kusoma weka alama zifuatazo kwenye matini unayosoma.**

**Weka alama ya mshangao (!) Kwenye wazo ambalo unadhani ni muhimu.**

**Weka alama ya kuuliza (?) Kuonesha kutokukubaliana na dhana hiyo.**

**Weka alama ya mduara (O) kuonesha kuwa dhana hiyo ni mpya kwako.”**

## DHANA KUU



### UMUHIMU WA UFAHAMU (DAKIKA 35)

1. Mwalimu mmoja aanze kusoma kwa sauti. Baada ya kukamilisha sehemu (kwa mfano, aya au maelezo) amwite mwalimu mwingine kwa jina asome sehemu inayofuata.
2. Wakati unaposoma zingatia alama zifuatazo:
  - Weka alama ya mshangao (!) katika sehemu ambayo unaona ni muhimu.
  - Weka alama ya kuuliza (?) katika sehemu ambayo huelewi au hukubaliani nayo.
  - Weka mduara katika (o) maneno ambayo ni mapya.

**Tunasoma ili kupata Ufahamu.** Wanafunzi wanapoelewa aya au matini, wanapokea sawasawa ujumbe unaowasilishwa. Hata hivyo, ni kawaida kwa wanafunzi kusoma au kusikiliza sentensi au hadithi na wasiweze kuelewa inamaanisha nini. Maswali ya aina tofauti tofauti yanayoulizwa kwa wanafunzi ni njia thabiti ya ya kukuza ufahamu kwasababu wanafunzi wanaongeza uelewa wao wanaposoma aya. Huu ndio uzoefu unaoupata wakati wa zoezi la Kuchangamsha. Mratibu wa Mafunzo aliwauliza aina tofauti za maswali ili kuwafanya muweze kushiriki kikamilifu katika aya mnayoisoma.

Ifuatayo ni orodha ya maswali ya kuwauliza wanafunzi kabla ya kusoma, wakati wa kusoma, na baada ya kusoma aya. Kumbuka, lengo la kuuliza haya maswali sio kuwapima wanafunzi, lakini ni kuwasaidia waweze kushiriki katika aya na kuinua ufahamu wao.

#### Maswali kabla ya kusoma:

**1. Gundua kile wanafunzi wanachojua kuhusiana na mada ya hiyo aya:** Kabla ya kusoma, tumia kichwa cha habari, picha na maneno muhimu kutoka katika aya kuuliza wanafunzi kuhusu mada hiyo. Kwa mfano, wakati wa Zoezi la Kuchangamsha, mratibu amewauliza: Taja jina la kiumbe katika kielelezo hiki? Je, ni aina gani za viumbe wa baharini una uzoefu nao? Kama picha na kichwa cha habari vinahusu ng'ombe, unaweza kuuliza: Huyu ni nani? Ng'ombe anaishi wapi? Ng'ombe analiaje? Je, ng'ombe ambao umeshawaona wana rangi gani?

**2. Angalia picha na ufundishe msamiati mpya:** Pitia picha za hiyo aya na uone kama wanafunzi wanajua msamiati unaohusiana na hizo picha. Kama sivyo, tumia picha KUFUNDISHA maneno mapya.

**3. Waulize wanafunzi watabiri kwamba hadithi inahusu nini:** Baada ya kujadili maneno muhimu au baada ya KUFUNDISHA maneno mapya, wanafunzi wakisie kwamba hadithi itakuwa inahusu nini. Kwa mfano, wakati wa Zoezi la Kuchangamsha, mratibu wa mafunzo ya walimu kazinin waulize: Je, mnafikiri matini hii itakuwa inahusu nini? Kama unajadili maneno "ng'ombe", "kwea" na "majani" wanafunzi waweza wakakisia hadithi hiyo. "Ng'ombe atakula majani" au "Ng'ombe atakwea kilima."

#### Maswali wakati wa kusoma:

**4. Uliza maswali yanayojenga kumbukumbu:** Haya ni maswali yanayohusu mambo yaliyotendeka katika hadithi. Kama vile, "Hadithi hii imefanyikia wapi? Nani mhusika mkuu katika hadithi? Kwa mfano, wakati wa Zoezi la Kuchangamsha, mratibu amewauliza: **Je, pweza ana mioyo mingapi? Je, ni mbinu gani ambazo pweza anazozitumia kujinasua kutoka katika hali ngumu? Je, pweza ana mikono mingapi?** Maswali haya yanaweza kujibiwa kama unaosikiliza hadithi au kuangalia picha. Ni muhimu kuwapa wanafunzi muda wa kujibu na kama hawana uhakika na jibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kwenye picha au maneno yaliyomo katika ukurasa utakaowaelekeza kwenye jibu.

## DHANA KUU



### WAAMBIE WALIMU:

**“Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”**

## DHANA KUU

**5. Uliza maswali yanayofikirisha:** haya ni maswali yanayowataka wanafunzi kufikiri zaidi ya maneno yaliyoandikwa katika ukurasa kuhusiana na hadithi. Mara nyingi haya ni maswali ya “kwanini” au “kwa jinsi gani”. Kwa mfano, wakati wa Zoezi la Kuchangamsha, mratibu amewauliza: **Kwanini unafikiri mbinu za kujinasua ni lazima kwa pweza? Kwanini unafikiri wana mikono mingi?** Maswali yanayofikirisha yanasaidia wanafunzi kuwa hodari na wasomaji makini. Wape wanafunzi muda zaidi wa kujibu haya maswali. Kama hawawezi kujibu, jaribu kuliuliza swali kwa namna ingine.

**Uliza maswali yanayohusisha uzoefu na mazingira:** jaribu kuhusianisha hadithi na maisha ya kila siku ya wanafunzi – kwa mfano, mratibu amewauliza: **Je, ni aina gani za viumbe wa baharini una uzoefu nao? Kama binadamu, unazo mbinu ambazo unazitumia kujinasua ukiwa katika hali ngumu? Je, ulishawahi kuona au kugusa pweza? Je, unajua wanyama wengine wowote walio na kiwango cha juu cha akili?** Maswali yanayohusisha uzoefu na mazingira.

**Maswali baada ya kusoma:**

**6. Uliza maswali ya nyongeza “yanayojenga kumbukumbu”, “yanayofikirisha” na “yanayohusisha uzoefu na mazingira”:** baada ya kusoma hadithi, uliza maswali yenye majibu mapana kuhusu mambo yaliyotendeka katika hadithi. Maswali ya kwanini/kwa jinsi gani na maswali yanayounganisha hadithi na maisha ya wanafunzi.

**7. Waambie wanafunzi wasimulie hadithi kwa maneno yao wenyewe:** baada ya kusoma, waambie wanafunzi wafupishe hadithi au aya kwa njia ya maelezo, mchezo wa kuigiza au mchoro. Kwa mfano, mratibu amewauliza: Je, unaweza kufupisha kwa sauti matini kwa maneno yako mwenyewe?

**8. Kadiria ufahamu wa wanafunzi katika hadithi:** uliza maswali yanayojenga kumbukumbu na maswali yanayofikirisha pamoja na kuwaambia wanafunzi waeleze hadithi kwa maneno yao wenyewe (ama kwa kuongea au kuandika aya fupi) kutakupatia wazo zuri zaidi la kujua kama wameelewa. Kama ukikuta wanafunzi hawaelewi vizuri aya, fikiria namna utakavyorekebisha maswali “kabla ya kusoma, wakati wa kusoma, na baada ya kusoma” ili kuinua kiwango cha ufahamu wa wanafunzi.

Maswali haya ya ufahamu yatanua kwa kina stadi za wanafunzi na kuwatia moyo kufikiri zaidi kuhusu kile walichosoma kuliko tu kukariri maneno. Hata hivyo, ni muhimu pia kwa walimu kutumia mikakati hii na aya ambazo zimeandikwa kufaa darasa kwa ajili ya hatua ya wanafunzi wao ya kukuza kusoma. Kwa kawaida makundi ya wanafunzi katika kusoma zinajulikana kama:

1. Wanaoibukia Kusoma
2. Wanaoanza Kusoma
3. Wasomaji wenye ufasaha wa awali
4. Wasomaji wenye ufasaha

Leleweke kuwa hatua hizi si lazima ziwe na uhusiano wa kiwango katika shule. Mfano, mwanafunzi wa darasa la pili anaweza kuwa mwenye kusoma kwa ufasaha na mwanafunzi wa darasa la saba akawa ndo anaibukia kusoma. Ikuatayo hapa chini ni jedwali lifuatalo linafanua makundi ya wanafunzi kwa kuzingatia uwezo wao wa kusoma matini au aya.. Kama wanafunzi watakuwa wanasoma matini au aya lengo ni kubaini wanafunzi wanaoweza kusoma aya au matini kwa usahihi kwa 90%. Kama mwalimu anawasomea wanafunzi kitabu kwa sauti, kitabu kinaweza kuwa cha hatua ya juu ili mradi mwalimu atatoa maswali yanayozingatia hatua ya “kabla ya kusoma, wakati wa kusoma, na baada ya kusoma” ili kuongeza ufahamu wa wanafunzi.

## DHANA KUU



### WAAMBIE WALIMU:

**“Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”**



### WAAMBIE WALIMU:

**“Sasa kila mwalimu atashirikisha wenzake kitu alichoonna ni muhimu, hakieleweki au kipya. Kisha tutajadili kwanini tunafikiri kusoma kwa sauti kutawasaidia wanafunzi wetu.”**

Eleza kila mwalimu atoe majibu yake. Kama walimu wanakwama juu ya swali la 4, hapa kuna jibu ambalo unaweza kuwashirikisha:

**Jibu 4:** Kuuliza aina tofauti za maswali ni njia thabiti ya kukuza ufahamu kwasababu wanafunzi wanaongeza uelewa wao wanaposoma kitabu.



## DHANA KUU

MAKUNDI	KILE MSOMAJI ANACHOWEZA KUFANYA:	SIFA ZA KITABU:
<b>Wanaoibukia Kusoma</b>	Wanaoibukia kusoma ndio tu wanaanza kushika dhana za msingi za kusoma vitabu na maandishi. Ndio wanaanza kuhusianisha sauti za herufi na herufi zilizoandikwa. Msamiati wao wa kuongea una nguvu zaidi ya ule wa maandishi, lakini wanaweza wakawa na uwezo wa kutambua baadhi ya maneno ambayo wanayaona mara kwa mara katika maandishi (kama vile kwa, na, mama, n.k). Wanategemea sana picha ili kuelewa kitabu.	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Maneno 4 au pungufu katika ukurasa</li> <li>• Maneno mengi mafupi</li> <li>• Maneno yanayojirudia</li> <li>• Picha kubwa inayowasilisha ujumbe</li> <li>• Maandishi makubwa</li> <li>• Vitendo na vitu vinavyojulikana</li> <li>• Usimuliaji wa hadithi sio lazima</li> <li>• Kitabu kiwe na kurasa 6-7</li> </ul>
<b>Wanaoanza Kusoma</b>	Wanaoanza kusoma wameshapata uelewa wa alfabeti, sauti za herufi na wanaweza kutumia ujuzi wao wa sauti za herufi kutengeneza maneno mapya. Wasomaji wanaoanza wanajua maneno mengi katika maandishi na wanaweza sasa kuyatambua bila kufikiri. (kama shule, pika, soma, nk.)	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Sentensi 2 mpaka 3 katika ukurasa</li> <li>• Muundo mgumu kidogo wa sentensi</li> <li>• Maneno mengi ya silabi 2-3</li> <li>• Baadhi ya maneno yenye silabi 4-6</li> <li>• Picha inayowasilisha ujumbe</li> <li>• Mada inayojulikana lakini ya kina zaidi</li> <li>• Anza na usimuliaji rahisi wa hadithi iwe kurasa 8-9</li> </ul>
<b>Wasomaji wenye ufasaha wa awali</b>	Katika hatua hii, wanaweza kusoma zaidi bila kufikiri, nguvu nyingi ikielekezwa kwenye ufahamu. Wanaona alama za uandishi, wanajua maneno mengi katika maandishi, na kutumia picha tu kuthibitisha uelewa wao wa aya. Wasomaji hawa wanahitaji kupata uzoefu wa aina mbalimbali za vitabu na wana uwezo mkubwa zaidi wa kutambua namna na aina mbalimbali za mitindo.	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Sentensi 4-5 katika ukurasa</li> <li>• Sentensi nyingi ndefu zaidi</li> <li>• Maneno mengi yenye silabi 4-6</li> <li>• Maneno mengi mapya</li> <li>• Hawategemei sana picha</li> <li>• Usimuliaji wa hadithi ni mgumu zaidi</li> <li>• Majibizano yanaweza kuwepo</li> <li>• Kitabu kiwe na kurasa 10-11</li> </ul>
<b>Wasomaji wenye ufasaha</b>	Wanaosoma kwa ufasaha wanaweza kusoma bila wenyewe bila kutumia juhudi kubwa. Wanaweza kusoma kwa kudhihirisha na kutumia vituo inavyostahili. Nguvu nyingi inaelekezwa katika uelewa na kutumia mikakati mbalimbali ya ufahamu.	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Vitabu vingi</li> <li>• Mada chache zinazojulikana</li> <li>• Maneno mapya yenye changamoto</li> <li>• Sentensi nyingi changamani.</li> <li>• Aina mbalimbali za mitindo ya uandishi</li> <li>• Maelezo mengi zaidi</li> <li>• Kitabu lazima kiwe na kurasa kuanzia 12 na kuendelea</li> </ul>

Baadae katika moduli hii, utaandika Kitabu chako Kikubwa cha kusoma kwa sauti darasani kwako. Kwa kuwa kitabu hiki kitakuwa chako cha kusoma kwa sauti darasani kwako, unaweza kutunga kitabu chako katika kiwango cha juu zaidi ya hatua ya ukuaji ya wanafunzi wako. Hakikisha tu unatumia maswali ya "kabla, wakati wa, na baada" ili kuendeleza ufahamu wa wanafunzi wako.



### FIKIRI – JOZISHA – SHIRIKISHANA (DAKIKA 10)

Jibu maswali ya fuatayo na mwenzako. Kisha mtashirikisha majibu yenu kwenye kikundi

1. Maudhui gani umewekea alama ya mshangao (!)?
2. Maudhui gani umewekea alama ya kuuliza (?)?
3. Maudhui gani umezungushia alama ya mduara?
4. Kwanini kuuliza wanafunzi maswali yanayohusu kitabu kunainua stadi zao za ufahamu?

## ZOEZI



### WAAMBIE WALIMU:

**“Sasa tutasoma kuhusu shughuli yetu ya leo ya mchezo wa kuigiza. Tutasoma maelekezo pamoja kwa sauti. Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma sehemu, wanaweza kuita jina la mwalimu mwingine ili asome sehemu inayofuata.”**

## ZOEZI




**IGIZO** (DAKIKA 30)

Igiza hadithi ifuatayo, mmoja awe mwalimu na wengine wawe wanafunzi kwa kuzingatia hatua zote tatu za kusoma kwa ufahamu tulizojifunza hapa juu. Sasa soma hadithi ifuatayo, na uandae maswali kisha umshirikishe mwenzako maswali uliyoandaa kwa ajili ya kuyaboresha.

### Timu ya Simba wameshinda mchezo!

Hadithi hii imetungwa na: **Bahati Temu**  
Mchoraji: **Marco Tibasima**



Siku moja, Mwalimu Kadio aliamua kucheza mchezo na wanafunzi wa darasa lake. Aliwagawa wanafunzi katika timu tatu. Timu hizo ziliitwa Simba, Chui na Tembo. Aliwaambia wanafunzi wake, "Kila timu itaanza na alama 100. Lakini kama nitaona mtu yeyote akicheza au kuongea wakati somo linaendelea, nitapunguza alama katika timu yake. Mwishoni mwa somo, timu itakayokuwa na alama nyingi itakuwa mshindi!" Mwalimu Kadio alianza kufundisha na wanafunzi wote walikuwa wema sana, lakini timu ya simba hawakupoteza hata alama moja! Simba walishinda mchezo na walikuwa na furaha sana!

## ZOEZI



### WAAMBIE WALIMU:

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

## ZOEZI

### Maswali ya kukuza ufahamu

Maswali kabla ya kusoma: (Uliza maswali haya kabla hujasoma hadithi kwa sauti)

**1. Baini kile ambacho tayari wanafunzi wanakijua kuhusu maudhui ya hadithi:** tumia kichwa cha habari, picha na maneno muhimu katika aya kuwauliza maswali wanafunzi kuhusu mada. Kwa mfano, "Ni aina ngapi za michezo mnayocheza shuleni?"

Andika swali: \_\_\_\_\_

**2. Angalia picha na ufundishe maneno mapya:** Onesha picha na angalia kama wanafunzi wanajua neno linalohusiana na picha. Kama hawajui, tumia picha KUFUNDISHA maneno mapya.

Chukua kitu halisi au picha ufundishie maneno mapya: \_\_\_\_\_

**3. Waambie wanafunzi wafikirie hadithi itahusu nini.** Baada ya kujadili maneno muhimu au KUFUNDISHA maneno mapya wape wanafunzi fursa ya wafikiri hadithi itahusu nini.

Je utaulizaje upate utabiri: \_\_\_\_\_

### Maswali Wakati wa Kusoma: (Pumzika kwenye vituo vinavyofaa wakati wa kusoma hadithi ili uweze kuuliza maswali)

**1. Maswali yanayojenga kumbukumbu:** Haya ni maswali yanayohusu ukweli au mambo yaliyotendeka katika hadithi. Kama vile, "Hadithi hii ilitokea mahali gani? Nani alikuwa mhusika katika hadithi?"

Andika swali la kuuliza: \_\_\_\_\_

**2. Maswali yanayofikirisha: haya ni maswali yanayohitaji mwanafunzi afikiri kuhusu hadithi zaidi za maneno yaliyoandikwa katika ukurasa.** Mara kwa mara haya ni maswali kama vile "kwanini?" au "kwa jinsi gani?", "kwanini unafikiri mhusika alifanya hivi?"

Andika swali la kuuliza: \_\_\_\_\_

**3. Maswali yanayohusisha uzoefu na mazingira:** jaribu kuhusisha hadithi na maisha ya kila siku ya wanafunzi, kitabu kingine ambacho wamewahi kukisoma au uelewa wa dunia wa wanafunzi. Kwa mfano, "Je mwalimu wako alishawahi kucheza mchezo kama huu darasani kwenu?"

Andika swali la kuuliza: \_\_\_\_\_

## ZOEZI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

## ZOEZI

### Maswali baada ya kusoma: (Uliza maswali haya baada ya kumaliza kusoma hadithi)

**1. Uliza maswali ya nyongeza “yanayojenga kumbukumbu”, “yanayofikirisha” na “yanayohusisha uzoefu na mazingira”:** uliza maswali yenye majibu mapana kuhusu ukweli au mambo yaliyotendeka katika hadithi, maswali ya kwanini/kwa jinsi gani na jinsi gani hadithi inaungana na maisha ya wanafunzi.

Andika swali la linalojenga kumbukumbu: \_\_\_\_\_

Andika swali la linalofikirisha: \_\_\_\_\_

Andika swali la linalohusisha uzoefu na mazingira: \_\_\_\_\_

**2. Waambie wanafunzi wasimulie hadithi kwa maneno yao wenyewe:** baada ya kusoma, waambie wanafunzi wafupishe hadithi au kitabu kwa njia ya maelezo, mchezo wa kuigiza au mchoro.

Je, utaulizaje upate ufupisho: \_\_\_\_\_

**3. Kadiria ufahamu wa wanafunzi wa hadithi:** ukiuliza maswali yanayojenga kumbukumbu na maswali yanayofikirisha, ikiwa ni pamoja na kuwaambia waelezee hadithi kwa maneno yao wenyewe (ama kwa kuzungumza au kuandika aya fupi) kutakupatia wazo zuri la kujua kama wameelewa.

### Wanafunzi wako walisemaje kuonesha kwamba wameelewa au hawakuelewa hadithi:

#### MAELEKEZO MUHIMU:

Sasa umemaliza kutayarisha maswali yako, wewe na mwenzako mnatakiwa kuigiza. Mmoja wenu atakuwa mwalimu na kusoma hadithi ya “Timu ya Simba wameshibnda mchezo” kwa sauti. Kumbuka kuuliza maswali mliyotayarisha kabda, wakati na baada ya kusoma hadithi.

Pia, kumbuka kutumia Mikakati ya Kusoma kwa Sauti tuliyojadili katika moduli ya 5:

- Hakikishakwamba kila mwanafunzi anakuona na kukusikia unaposoma.
- Elekeza kidole kwenye kila neno unalolisoma.
- Soma kwa uwazi na hasia.

Baada ya kila mmoja kumaliza kuigiza kama mwalimu, na kuuliza maswali waliyoandika, kila mmoja arudi katika kikundi chake kwa majadiliano.



#### JADILI NA KIKUNDI (DAKIKA 10)

Mara baada ya kumaliza mchezo wa kuigiza, jadili maswali yafuatayo na kikundi:

- Kitu gani kilikuwa changamoto kuhusu kutengeneza maswali ya ufahamu?
- Je, utafanya nini kama wanafunzi wanashindwa kujibu maswali?
- Ni kwa jinsi gani utahakikisha kwamba kila mwanafunzi anapata nafasi ya kujibu maswali?

## KUPANGA MKAKATI



### WAAMBIE WALIMU:

**“Sasa tutapanga vipindi vyetu vya kusoma na kuandika. Tutasoma maelekezo pamoja na kwa sauti. Baada ya mwalimu wa kwanza kusoma sehemu, utamwita mwalimu mwingine kwa jina ili asome sehemu inayofuatia.”**



## KUPANGA MKAKATI



### KUAANDAA KIPINDI CHA “KUSOMA NA KUANDIKA” (DAKIKI 15)

Ili kukuza uwezo wa wanafunzi kusoma, ni muhimu sana kwamba aweze kufanya mazoezi juu ya mbinu mpya za kusoma na kuandika alizosoma kutoka kwenye Mafunzo ya Walimu Kazini.

Kurasa zifuatazo zinajumuisha masomo ya jumla yanayoelekeza shughuli ambazo unaweza kujaribu wakati wa kipindi chako cha kusoma na kuandika (au unaweza pia kujaribu wakati wa kipindi chako cha kawaida cha Kiswahili). Pamoja na mwenzako:

1. Soma kwenye mpango wa masomo.
2. Jaza nafasi zilizo wazi mahali panapohitaji hivyo.
3. Jaribu masomo wakati wa kipindi cha kusoma na kuandika.

### MWONGOZO WA SOMO LA KWANZA: Maswali ya Ufahamu HATUA ZA UFUNDISHAJI

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
<b>MATAYARISHO</b>	<ol style="list-style-type: none"><li>1. Kabla ya kipindi, soma tena hadithi ya ‘Timu ya Simba wameshinda mchezo’.</li><li>2. Tayarisha maswali angalau matatu ya ‘kabla, wakati wa, na baada’ ambayo utawauliza wanafunzi wako. Unaweza kutumia baadhi ya maswali uliyoandaa wakati wa mchezo wa kuigiza: <b>Maswali kabla ya kusoma:</b><ol style="list-style-type: none"><li>1. Gundua kile ambacho tayari wanafunzi wanakijua kuhusu mada ya kwenye kitabu: tumia kichwa cha habari, picha na maneno muhimu kutoka katika kitabu uulize wanafunzi kuhusu mada ya hadithi. Andika maswali ya kuuliza:<ul style="list-style-type: none"><li>• _____</li><li>• _____</li><li>• _____</li></ul></li><li>2. Angalia picha na ufundishe maneno mapya: Chukua vitu halisi vitatu au picha ufundishe maneno mapya:<ul style="list-style-type: none"><li>• _____</li><li>• _____</li><li>• _____</li></ul></li><li>3. Waambie wanafunzi watabiri kwamba hadithi inahusu nini. Baada ya kujadili maneno muhimu au KUFUNDISHA maneno mapya, wanafunzi wapate fursa ya kufikiria hadithi itahusu nini: _____</li></ol></li></ol>

## KUPANGA MKAKATI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

## KUPANGA MKAKATI

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
<b>MATAYARISHO</b>	<p><b>Maswali wakati wa kusoma:</b></p> <p>1. Maswali yanayojenga kumbukumbu : haya ni maswali yanayohusu ukweli au mambo yaliyotendeka katika hadithi. Andika maswali matatu:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• _____</li> <li>• _____</li> <li>• _____</li> </ul> <p>2. Maswali yanayofikirisha : Mara kwa mara haya ni maswali ya “kwanini” au “kwa jinsi gani?”. Andika maswali matatu:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• _____</li> <li>• _____</li> <li>• _____</li> </ul> <p>3. Maswalik yanayohusisha uzoefu na mazingira : jaribu kuhusianisha hadithi na maisha ya kila siku ya wanafunzi, kitabu kingine walichowahi kusoma au uelewa wao wa dunia. Andika maswali matatu:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• _____</li> <li>• _____</li> <li>• _____</li> </ul> <p><b>Maswali baada ya kusoma:</b></p> <p>1. Uliza maswali ya nyongeza ya “yanayojenga kumbukumbu”, “yanayofikirisha” na “yanayohusisha uzoefu na mazingira”:</p> <p>Andika swali linalojenga kumbukumbu: _____</p> <p>Andika swali linalofikirisha: _____</p> <p>Andika swali linalohusisha uzoefu na mazingira: _____</p> <p>_____</p> <p>2. Waambie wanafunzi wasimulie hadithi kwa maneno yao wenyewe: baada ya kusoma, waambie wanafunzi wafupishe hadithi kwa maneno yao wenyewe. Ondoa sio sehemu ya hatua za somo</p>
<b>UTANGULIZI</b>	<p>1. Waambie wanafunzi kwamba unaenda kuwasomea hadithi. Utawauliza maswali yanayohusu hadithi hiyo na ungependa wajitahidi kwa kadri wawezavyo kujibu maswali hayo.</p>

## KUPANGA MKAKATI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

## KUPANGA MKAKATI

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
<b>KUJENGA UMAHIRI</b>	2. Anza na maswali kabla ya kusoma ambayo umeyaandaa.
<b>KUTUMIA UMAHIRI</b>	3. Anza kusoma hadithi kwa sauti na kuanza kuuliza maswali ya wakati wa kusoma ambayo umeyaandaa. 4. Baada ya kumaliza kusoma hadithi, uliza maswali ya baada ya kusoma ambayo umeyaandaa. 5. Waambie wanafunzi waigize hadithi: gawanya wanafunzi katika makundi ya 4-5 (unaweza kuwaweka wanaoshirikiana dawati pamoja, lakini pia jaribu kuweka jozi za wanafunzi wenye uwezo mkubwa na wale wenye uwezo mdogo). 6. Wape wanafunzi nafasi ya kuigiza tukio lililotokea mwanzoni mwa hadithi, katikati na mwishoni.
<b>KUPIMA</b>	7. Tafakari majibu ya wanafunzi ya maswali ya "juu juu" na "kina", pamoja ufupisho wa wanafunzi na maigizo yao. 8. Ikiwa utagundua kwamba wanafunzi hawaelewe kitabu, fikiri jinsi utakavyorekebisha maswali ya "kabla ya kusoma, wakati wa kusoma na baada ya kusoma" ili kuinua ufahamu wa wanafunzi.

Tathmini ya Ufundishaji: \_\_\_\_\_

Tathmini ya Ujifunzaji: \_\_\_\_\_

Maoni: \_\_\_\_\_

## KUPANGA MKAKATI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

## KUPANGA MKAKATI

### MWONGOZO WA SOMO LA PILI: Namna tofauti ya kumalizia hadith HATUA ZA UFUNDISHAJI

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
<b>MATAYARISHO</b>	<p>Kabla ya siku ya somo, chagua hadithi utakayosoma. Kama umepokea vitabu vya kiada vya EQUIP-Tanzania, chukua kitabu kinachofaa kwa darasa lako. Kama huna vitabu hivi, unaweza tena kutumia hadithi ya 'Neema haogopi'. Jisomee hadithi wewe mwenyewe na uandae maswali ya 'kabla, wakati wa, na baada' ambayo utauliza wakati wa kusoma hadithi:</p> <p><b>Maswali kabla ya kusoma:</b></p> <p>1. Gundua kile wanafunzi wanachojua kuhusiana na mada ya hiyo aya: tumia kichwa cha habari, picha na maneno muhimu kutoka katika aya uwaulize wanafunzi kuhusu mada ya hadithi. Andika maswali matatu ya kuuliza:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• _____</li> <li>• _____</li> <li>• _____</li> </ul> <p>2. Angalia picha na ufundishe maneno mapya: Chukua vitu halisi vitatu au picha ufundishe maneno mapya:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• _____</li> <li>• _____</li> <li>• _____</li> </ul> <p>3. Waambie wanafunzi wafikirie hadithi inahusu nini. Baada ya kujadili maneno muhimu au KUFUNDISHA maneno mapya, wape wanafunzi fursa ya kufikiri hadithi itakuwa inahusu nini:</p> <p>_____</p> <p><b>Maswali wakati wa kusoma:</b></p> <p>4. Maswali yanayojenga kumbukumbu : haya ni maswali yanayohusu ukweli au mambo yaliyotendeka katika hadithi. Andika maswali matatu:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• _____</li> <li>• _____</li> <li>• _____</li> </ul> <p>5. Maswali yanayofikirisha : Mara kwa mara haya ni maswali ya "kwanini" au "kwa jinsi gani?". Andika maswali matatu:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• _____</li> <li>• _____</li> <li>• _____</li> </ul> <p>6. Maswalik yanayohusisha uzoefu na mazingira : jaribu kuhusianisha hadithi na maisha ya kila siku ya wanafunzi, kitabu kingine walichowahi kusoma au uelewa wao wa dunia. Andika maswali matatu</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• _____</li> <li>• _____</li> <li>• _____</li> </ul>

## KUPANGA MKAKATI

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)



## KUPANGA MKAKATI

HATUA	SHUGHULI ZA KUFUNDISHIA
<b>MATA-YARISHO</b>	<p><b>Maswali baada ya kusoma:</b></p> <p>1. Uliza maswali ya nyongeza “yanayojenga kumbukumbu”, “yanayofikirisha” na “yanayohusisha uzoefu na mazingira”:</p> <p>Andika swali linalojenga kumbukumbu: _____</p> <p>Andika swali linalofikirisha: _____</p> <p>Andika swali linalohusisha uzoefu na mazingira: _____</p> <p>2. Waambie wanafunzi wasimulie hadithi kwa maneno yao wenyewe: baada ya kusoma, waambie wanafunzi wafupishe hadithi kwa maneno yao wenyewe.</p> <p>Sehemu hapa sio mahali pake na wala sio sehemu ya hatua za somo-ondoa</p>
<b>UTANGULIZI</b>	Waambie wanafunzi kwamba utawasomea hadithi. Utawauliza maswali yanayohusu hadithi hiyo na ungependa wajitahidi kwa kadri wawezavyo kujibu maswali hayo.
<b>MAARIFA MAPYA</b>	1. Anza na maswali ya kabla ya kusoma ambayo umeyaandaa.
<b>KUKAZIA</b>	1. Anza kusoma hadithi kwa sauti na uanze kuuliza maswali ya wakati wa kusoma ambayo umeyaandaa.
<b>MAZOEZI</b>	<p>1. Baada ya kumaliza kusoma hadithi, uliza maswali ya baada ya kusoma ambayo umeyaandaa.</p> <p>2. Waambie wanafunzi waigize hadithi: gawanya wanafunzi katika makundi ya 4-5 (unaweza kuwaweka wanaoshirikiana dawati pamoja, lakini pia jaribu kuweka jozi za wanafunzi wenye uwezo mkubwa na wale wenye uwezo mdogo).</p> <p>3. Wape wanafunzi nafasi ya kuigiza tukio lililotokea mwanzoni mwa hadithi, katikati na mwishoni. Lakini badala ya kuigiza tukio la sehemu ya mwisho ya hadithi, waambie wanafunzi waeleze namna mpya ya umalizaji wa hadithi.</p>
<b>KUPIMA</b>	<p>1. Tafakari majibu ya maswali ya wanafunzi ya “juu juu” na “kina”, pamoja na ufupisho wa wanafunzi na maigizo.</p> <p>2. Ukikuta kwamba wanafunzi hawaelewi kitabu, fikiria kuhusu jinsi utakavyorekebisha maswali ya “kabla, wakati wa, na baada” ili kuinua ufahamu wa wanafunzi.</p>
Tathmini: _____	
Maoni: _____	

## UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHA



### WAAMBIE WALIMU:

**“Sasa tunaenda kusoma kuhusu zana ya kufundishia ambayo tunaweza kuitumia kuwasaidia wanafunzi kukuza stadi za ufahamu wao. Inaitwa kitabu kikubwa. Hebu tupokezane kusoma sehemu hii kwa sauti. Baada yakusoma, kila mmoja atafanya kazi mwenyewe ya kupanga kitabu chake kikubwa. Niko hapa kujadiliana nanyi kama mnahitaji msaada.”**

## UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHA



### MAANDALIZI YA KUANDIKA KITABU KIKUBWA (DAKIKA 30)

Vitabu vikubwa ni vitabu vya hadithi ambavyo vina picha na maneno makubwa. Vitabu hivyo vinafaa kwa wanafunzi kusoma kwa sauti madarasani kwao kwa sababu picha na maneno makubwa huwarahisishia wanafunzi kuona na kufuatilia hadithi hasa kwa madarasa makubwa. Leo, utaandika kitabu na kubuni picha kwa ajili ya kitabu chako kikubwa. Wakati wakusoma moduli ifuatayo ya 13, utaanza kutengeneza kitabu chako kikubwa.



#### HATUA YA 1:

**Amua hatua ya ukuaji wa kusoma wa darasa lako** Kabla ya kuanza kuandika kitabu chako kikubwa, unahitaji kufikiria juu ya hatua ya ukuaji wa kusoma ambayo wanafunzi wako wamefikia. Wanafunzi wako katika kundi gani?

1. Wanaoibukia Kusoma
2. Wanaoanza Kusoma
3. Wasomaji wenye ufasaha wa awali
4. Wasomaji wenye ufasaha

Tafadhali pitia chati uliyosoma katika dhana za msingi na uweze kuamua hatua ya wasomaji darasani kwako. Kisha uangalie maneno ya vitabu ambayo yanafaa kwa ajili ya hatua hiyo. Tumia hizo picha kukuongoza kuandika maneno yako ya kitabu kikubwa. Kwakuwa utakuwa ukisoma kitabu kikubwa kwa wanafunzi wako kwa sauti, unaweza pia kutunga kitabu chako kiwe katika kiwango cha daraja la juu ili mradi utoe maswali ya "kabla, wakati wa, na baada" ili kuendeleza ufahamu wa wanafunzi. Kwa mfano, kama mwalimu wa darasa la 1 ana wasomaji wengi wanaoibukia darasni kwake, anaweza kuchagua kuandika kitabu kikubwa chenye maneno kwa ajili ya wasomaji wanaoanza:

- Sentensi 2 mpaka 3 katika ukurasa
- Sentensi nyingi zaidi zenye muundo changamano
- Maneno mengi yenye silabi 2-3
- Baadhi ya maneno yenye silabi 4-6
- Picha inayowasilisha ujumbe
- Mada zinazofahamika lakini zenye maarifa mapana zaidi
- Anzia na usimuliaji rahisi wa hadithi
- Kitabu kitakuwa na kurasha 8-9

Hata hivyo, ni vizuri kabisa kutunga kitabu chenye sifa zinazoendana na kiwango cha hatua ya darasa lao. Chaguo ni lako.

#### HATUA YA 2:

**Chagua mada au hadithi ya kitabu chako kikubwa** Kitabu kikubwa kitalenga kwenye mada hiyo inayoburudisha na inayohusiana na maisha ya wanafunzi. Kwa mfano:

- Kile wanafunzi wanachofanya wakati wa mchana wakiwa shuleni
- Vyakula wanafunzi wanavyokula na familia zao
- Hisia zilizozoeleka kwa watoto (msisimko, wivu, hofu) na hali za kawaida ambazo zinaweza kumfanya mwanafunzi ajisikie hivyo
- Mada zinazohusiana na muhtasari wa Kiswahili. Kwa mfano, darasa la 1 – Salamu, Utambulisho, Rangi. Darasa la 2 – Wanafamilia, umoja/wingi. Darasa la 3 – Maeneo ninayotembelea, viwango vya vitu.
- Mada zinazohusiana na maneno mapya ambayo umefundisha au utakayofundisha

**HATUA YA 3: Andika maneno na sentensi kwa kila ukurasa na uamue picha utakazotumia** Wakati umeshachagua mada yako, tumia karatasi hii ya kitabu kikubwa kupanga kitabu chako na picha (si lazima utumie kurasa zote – tumia tu idadi inayofaa kwa darasa lako). Karatasi hii inakupa nafasi ya kuandika maneno pamoja na kuchora aina ya mchoro unaopelekana na kitabu chako. Kila picha ioneshe wazo kuu au maneno mapya tofauti yaliyomo kwenye kitabu. Usijali kama huwezi kuchora! Haya sio mashindano ya kuona nani ni msanii bora wa kuchora. Fanya kwa kadri uwezavyo – wanafunzi watafurahi kuona aina yoyote ya mchoro.

## UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHA

(Zunguka na uliza ikiwa walimu wanahitaji msaada)

## UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHA

Mada: \_\_\_\_\_ Mwandishi: \_\_\_\_\_

<p>Ukurasa 1: Makala</p> <p>Mchoro:</p>	<p>Ukurasa 2: Makala</p> <p>Mchoro:</p>	<p>Ukurasa 3: Makala</p> <p>Mchoro:</p>
---	---	---

<p>Ukurasa 4: Makala</p> <p>Mchoro:</p>	<p>Ukurasa 5: Makala</p> <p>Mchoro:</p>	<p>Ukurasa 6: Makala</p> <p>Mchoro:</p>
---	---	---

<p>Ukurasa 7: Makala</p> <p>Mchoro:</p>	<p>Ukurasa 8: Makala</p> <p>Mchoro:</p>	<p>Ukurasa 9: Makala</p> <p>Mchoro:</p>
---	---	---

## UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHA



### WAAMBIE WALIMU:

**“Tunaendelea kusoma matini kwa sauti na kwa kupokezana.”**

## UTENGENEZAJI WA ZANA ZA KUFUNDISHA



### UFUATILIAJI

Baada ya kumaliza moduli hii, Afisa Elimu Kata, Afisa Elimu wa Wilaya na Mkaguzi wa Wilaya watafuatilia ili waone jinsi unavyotumia mikakati iliyopo kwenye moduli hii darasni kwako. Wakati huu wa ufuatiliaji, itakuwa vyema kuweza kuonesha wazi yafuatayo:

- a) Toa mifano ya maswali utakayouliza 'kabla ya kusoma'
- b) Toa mifano ya maswali utakayouliza 'wakati wa kusoma'
- c) Toa mifano ya maswali utakayouliza 'baada ya kusoma'
- d) Onesha karatasi ya kazi ya Kitabu Kikubwa ulichotengeneza.
- e) Onesha wazi jinsi ulivyotumia maandalio yako ya somo kutokana na moduli hii darasani kwako.

## MWISHO



### WAAMBIE WALIMU:

**“Walimu, tumefika mwisho wa moduli yetu, tumia dakika kumi kutafakari somo letu la leo. Jaza fomu kurekodi tathmini yako ya moduli. Baada ya kukamilisha chomoa ukurasa huo unipatie. Tafadhali uwe mkweli katika majibu yako kwa sababu yatasaidia kuboresha Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule hapo baadaye.”**

Kusanya fomu za tathmini zilizokamilishwa na walimu na uwe nazo wakati wa mkutano mwingine katika kundi la kata.

Wakati walimu wanaendelea kujaza fomu za tathmini, tafadhali tafakari kwa ujumla juu ya mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha siku hiyo na jaza visanduku vinavyofuata. Haya utaweza kuyajadili pamoja na Timu ya Wilaya ya Mafunzo Walimu Kazini na Waratibu wengine wa Mafunzo Walimu Kazini wa mkutano unaofuata katika kundi la kata.

MAFANIKO YA JUMLA YA KIPINDI HIKI:	CHANGAMOTO ZA JUMLA ZA KIPINDI HIKI:
Shule: _____ Wilaya: _____ Mkoa: _____	
Tafakuri za Moduli # _____ Mada ya Moduli: _____	
Idadi ya walimu walioshiriki : _____ Mwalimu Mkuu alishiriki : Ndiyo/Hapana	



## MWISHO



### MWISHO (DAKIKA 10)

Binafsi jaza fomu ifuatayo kuweka rekodi ya tathmini ya moduli ya leo. Baada ya kukamilisha, chomoa ukurasa huu na umpe Mratibu wako. Tafadhali uwe mkweli kwa vile mrejesho wako utasaidia kuboresha Mafunzo ya Walimu Kazini ngazi ya shule hapo baadaye.

### JEDWALI LA KUTATHMINI

Alama 0: Sikubaliani kabisa na usemi huu	Alama 1: Kwa kiasi Sikubaliani na usemi huu	Alama 2: Nakubaliana kwa kiasi na usemi huu	Alama 3: Nakubaliana Kabisa na usemi huu
--	---	---	--

### FOMU YA TATHMINI

Shule: \_\_\_\_\_ Wilaya: \_\_\_\_\_ Mkoa: \_\_\_\_\_

Tathmini ya Moduli: \_\_\_\_\_ Mada ya Moduli: \_\_\_\_\_

Idadi ya walimu walioshiriki: \_\_\_\_\_ Mwalimu Mkuu alishiriki: Ndiyo/Hapana

Mratibu alikuwepo kuwezesha: Ndiyo/Hapana

Soma semi zifuatazo kisha weka alama ya vema katika kisanduku husika kuonesha jibu lako:	0	1	2	3
1. Dhana kuu ya moduli ya leo ilikuwa inaeleweka.				
2. Moduli hii ina mikakati mingi mizuri na yenye manufaa ambayo nitaitumia darasani kwangu.				
3. Muda uliotumika kukamilisha moduli hii unafaa. Sikuhisi kwamba ni muda mrefu sana.				
4. Moduli hii iliibua mjadala wa kufurahisha na tafakuri ya hali ya juu sana.				
5. Violezo vya kipindi cha kusoma na kuandika vilisaidia sana. Natarajia vitakuwa rahisi kuvitumia ndani ya darasa langu.				
6. Zana tulizotengeneza leo zitakuwa za manufaa sana (kama inahusika).				
7. Mratibu amejiandaa kwa kipindi – amesoma vizuri moduli na ameandaa vifaa vyote vya kufundishia.				
8. Mratibu anasimamia vizuri majadiliano – anajua jinsi ya kuwafanya watu wajieleze na namna ya kupata majibu.				
9. Mratibu anajua namna ya kusimamia makundi – anahakikisha kuwa walimu wanatoa ushirikiano, wanashirikiana na wana hamasika.				
10. Mratibu anajua jinsi ya kuwahamasisha walimu – anafuatilia kujua waliokosa vipindi au kuchelewa na kutukumbusha kwanini Mafunzo ya Walimu Kazini ni muhimu kwetu.				





